JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFSI YA RAIS   TAWALA ZA MIKOA   NA SERIKALI ZA MITAA

MWONGOZO WA USAHISHAJI MTIHANI WA KISWAHILI 1

SHULE ZA VIPAJI MAALUMU

KIDATO CHA SITA

121/1 MACHI 2024

---

1.

a. UFISADI UNAOFANYWA NA WANAWAKE
UFISADI WA WANAWAKE KATIKA JAMII

b. i. Vimulimuli- wanawake wanaowaka/wazuri/wanaopendeza
ii. Kimuyemuye-wasiwasi
iii. Honoraria-malipo ya hiari
iv. Akajinasibu-akajitambua
v. Ukiritimba-kujilimbikizia mali/bila ya kuwajali wengine

c. Madhara ya ufisadi
-kurudisha nyuma maendeleo
-huchochea ukandamizaji
-hupelekea kukosa kwa haki katika jamii
-kuleta ukiritimba uliopitiliza

d. Katika haya ya sita mwandishi anamaanisha kuwa kuwepo kwa ufisadi uliopitiliza katika jamii hupelekea jamii kukosa maendeleo na ufisadi huo usipopingwa kwa nguvu na kung'olewa jamii haitapata maendeleo.

a=01
b.@1=
c. @1=
d= 01
Jumla

2. Tofauti zilizopo kati ya mofimu na silabi

i. Tofauti katika maana

Mofimu ni kipashio kidogo cha kiisimu chenye maana kisarufi na kilekisika

Mfano baba- mofimu huru

Aliyechezewa – a-li-ye-chez-ew-a- mofimu tegemezi

Silabi ni sehemu ya neno inayotamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti

Mfano kaka- ka+ka

ii. Tofauti katika aina

Mofimu hugawanyika katika aina mbili; mofimu huru na mofimu tegemezi

Silabi hugawanyika katika aina mbili; silabi huru na silabi funge

iii. Tofauti katika kazi zake kisarufi

Mofimu hasa mofimu tegemezi katika tungo huwa na kazi maalumu kisarufi mfano, katika neno analima- **a-na**-lim-a, huonesha nafsi ya tatu umoja, njeo/ wakati uliopita mtawalia

Lakini si kila silabi katika tungo huwa na kazi maalumu kisarufi. Mfano katika neno baba- ba+ba silabi hizi hazina kazi maalumu kisarufi

iv. Mofimu hazivunji au kuugawa mzizi wa neno katika neno.

Mfano mofimu huru katika maneno kama **shangaz**i- huwa ni mzizi huru hivyo hauvunjwi lakini katika silabi neno s**hangazi** huvunjwa vunjwa mfano sha+nga+zi.

Pia katika mofimu tegemezi mzizi hauvunjwi. Mfano katika neno anampigia- a-na-m-**pig**-i-a, silabi katika neno hili huvunja na kuugawa mzizi wa neno mfano, a+na+m+pi+gi+a

v. Mofimu hasa mofimu tegemezi huwa na viambishi awali na tamati.

Mfano katika neno tuliyemchezea**- tu-li-ye-m-viambishi awali,**
**e-a- viambishi tamati.**

Lakini silabi katika neno hazina viambishi awali na tamati. Mfano katika neno hilo huwa **tu+li+ye+m+che+ze+a.**

vi. Mara nyingi katika mofimu hasa mofimu huru kuna idadi ndogo ya mofimu. Kwa mfano katika neno Kalamu-ni mofu huru moja lakini katika silabi neno hilo lina silabi tatu, ka+la+mu.

Hoja 4@ 02
Jumla 08

3.

i. Umilisi wa lugha ni ujuzi au uelewa wa kanuni zinazotawala lugha Fulani ambazo kila mzungumzaji wa lugha asilia huwa nazo
Mfano
Matamshi sahihi ya maneno
Mpangilio sahihi wa maneno katika sentensi

ii. Chagizo ni sehemu ya kiarifu katika sentensi ambayo hukaliwa na kielezi.
Mifano
Mama anasoma kitabu **taratibu taratibu**
Wanafunzi wameenda **shuleni**
Walimu wetu huamka **mapema alfajiri**

iii. Uambishaji wa kisarufi ni uambishaji ambao uamilifu wake ni kupachika viambishi vyenye kazi za kisarufi kwenye mzizi na uambishaji huu haubadlishi kategoria ya neno.
Mifano
a-na-lim-i-a
a-na-cho-ki-pig-a
a-li-ye-m-chez-e-a

iv. O-rejeshi ni kiambishi cha mtenda au mtendwa ambapo hujitokeza katika kitenzi au -amba- ili kuonesha dhana ya urejeshi au ni urejeshi unaofata mfumo wa upatanisho wa kisarufi.
O-rejeshi huweza kuaiishwa kwa kuwepo maumbo ya o-rejeshi na kiamishi –amba-
Mfano.
Anavyokula ananitamanisha
Mtoto aliyekuja ameondoka
Kiti kilichotengenezwa kimeuzwa
Ugonjwa uliozuka umetibika

v. Kitenzi kishirikishi haya ni maneno yanayoonesha tabia au hali fulani iliyopo au isiyokuwepo kwa kitu au mtu fulani
Mifano
Yeye **si** mchoyo
Mwalimu **alikuwa** mgonjwa
Watoto **ndio** wasumbufu
Mama **ni** mkarimu

**Hoja 5@ 02**
**Jumla 10**

4. Mambo yanayoweza kupelekea mtu kuwa mlumbi wa lugha

i. Biashara
ii. Hama hama ya watu
iii. Elimu
iv. Dini
v. Matumizi makubwa ya sayansi na teknolojia
vi. Kuoleana
vii. Ukoloni

**Hoja 5@ 02**
**Jumla 10**

5. Katika sehemu ya utangulizi mtahiniwa atoe fasili ya tafsiri na ukalimani

   Katika sehemu ya kiini mtahiniwa aeleze kwa mifano mbinu sita za kutathmini matini

   i. Ulinganishaji wa matini

      Hii ndiyo mbinu kongwe zaidi na ndiyo inayotumiwa na wahakiki wengi zaidi (MC na ML). Katika mbinu hii kinachofanyika ni kwamba matini lengwa hulinganishwa na matini chanzi ili kubaini vipengele vya kimuundo na kimtindo vilivyoongezwa, vilivyopunguzwa au vilivyopotoshwa ili kuvifanyia marekebisho.

   ii. Tafsiri rejeshi

      Ni mchakato wa kutafsiri matini ambayo tayari imetafsiriwa katika lugha fulani yaani lugha lengwa na kuirejesha tena katika lugha chanzi kwa lengo la kuitathmini tafsiri hiyo.

   iii. Kupima uasili

      Tafsiri bora haipaswi kusomeka kama tafsiri. Hii ina maana kwamba mtu anaposoma tafsiri yako asijue kama ni kazi iliyotafsiriwa badala yake inatakiwa isomeke kama vile imeandikwa katika lugha lengwa hiyohiyo. Hali ambapo tafsiri husomeka kama vile imeandikwa katika lugha lengwa hiyohiyo ndio ambayo huitwa uasili. Hapa mfasiri mwenyewe au mtu mwingi anaisoma kazi hiyo. Inashauriwa apewe mtu mwingine tena bila kuambiwa kwamba kazi hiyo ni tafsiri.

   iv. Kupima uelewekaji

      Katika mbinu hii kinachoangaliwa ni kueleweka kwa maudhui yanayotolewa katika tafsiri hiyo. Mtu anayepima uelewekaji atajiuliza yeye mwenyewe, je maudhui katika kazi hii yataeleweka kwa wasomaji au kazi hii inazungumzia nini? Hivyo inashauriwa kwamba mfasiri ampe mtu mwingine ili kuepuka kujipendelea. Tahadhari: Mtu anayepelekewa kazi hiyo inashauriwa awe mfasiri.

   v. Kupima usomekaji

Katika mbinu hii ya kupima usomekaji mfasiri au mhakiki atapima tafsiri husika ili kuona iwapo inasikika vizuri masikioni mwa msikilizaji na kama inamtiririko unaokubalika katika lugha lengwa. Hapa kunakuwa na watu wawili mmoja anasikiliza na mwingine anasoma kwa sauti.

vi. Kupima ulinganifu

Katika hii mhakiki anaangalia umakini wa mfasiri katika kutumia kwa namna inayofaa vipengele muhimu vya matini kama vile msamiati, istilahi, maudhui au maneno muhimu yanayobeba maudhui. Maana yake ni kwamba kama neno limejirudia rudia katika tafsiri usibadilishe, mfano: Aim – nia, lengo, madhumuni, kusudi, azma, shabaha, kusudi nk. Hivyo kama neno “Aim” umelifasiri kama lengo basi popote litakapojitokeza kwa mara nyingine katika matini basi libaki hivyohivyo bila kubadili badili.

Mtahiniwa katika sehemu ya hitimisho atoe hitimisho la kazi yake

Utanguli
Kiini hoja 6(
Hitimish
Jumla

6. Mtahiniwa aandike insha kwa kufuata kanuni na taratibu za uandishi wa insha
   i. Kichwa cha insha ,kiandikwe mwanzoni kabisa na kiandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari
   ii. Utangulizi wa insha
   iii. Katika kiini cha insha mtahiniwa afafanue kwa hoja zake zenye mashiko umuhimu wa mtaala mpya wa elimu nchini Tanzania
      a. Kuendana na Mahitaji ya Sasa
         Mtaala mpya huundwa ili kukidhi mahitaji ya kisasa na mabadiliko ya jamii, teknolojia, na uchumi. Hivyo, inahakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu inayoweza kuwawezesha kushiriki katika ulimwengu wa leo

      b. Kuboresha Ubora wa Elimu
         Mara nyingine, mtaala mpya unaweza kuleta maboresho katika njia za kufundisha na kujifunza, kuhakikisha kwamba elimu inakuwa ya ubora zaidi. Hii inaweza kujumuisha mbinu mpya za kufundisha, rasilimali, na mbinu za tathmini.

      c. Kuwajengea Wanafunzi Uwezo wa Kujifunza wa Maisha
         Mtaala mpya unaweza kujumuisha mbinu za kufundisha ambazo huwawezesha wanafunzi kujifunza kwa njia endelevu na kuendeleza uwezo wa kujifunza wa maisha.

      d. Kukidhi Mahitaji ya Soko la Ajira

Mtaala unaweza kubuniwa ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira, kwa kutoa wanafunzi stadi na ujuzi unaohitajika katika mazingira ya kazi

e. Ubunifu na Uvumbuzi
Kukuza ubunifu na uvumbuzi kupitia mtaala kunaweza kusaidia kujenga kizazi cha watu wenye uwezo wa kutatua changamoto za kisasa.

f. Kukuza elimu jumuishi
Mtaala unaweza kusisitiza elimu jumuishi, kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata fursa sawa za kujifunza, pamoja na wale wenye mahitaji maalum

g. Kukuza utaalamu wa teknolojia na Digitali.
Kuingiza teknolojia na ujuzi wa kidigitali katika mtaala kunaweza kuandaa wanafunzi kwa matumizi ya teknolojia katika maisha yao ya kila siku na kazi zao.

**Mtahiniwa anaweza kutoa hoja nyingine zinazokidhi matakwa ya swali.**

iv. Mwisho wa wa insha au hitimisho, mtahiniwa anaweza kutoa maoni au mapendekezo

**Kichwa cha insha 02**
**Utangulizi wa insha 01.**
**Kiini hoja 5@ 03=15**
**Hitimisho 01.5**
**Jumla 20**

7. Mtahiniwa atoe fasili ya lahaja katika sehemu ya utangulizi
Katika sehemu ya kiini mtahiniwa afafanue kwa mifano mambo yanayosababisha kutokea kwa tofauti katika kutumia lugha kuu moja
   i. Utengano wa kijiografia
   ii. Tofauti za kimatabaka
   iii. Upangaji wa lugha
   iv. Kupita kwa wakati
   v. Uwepo wa mitindo binafsi
   vi. Hama hama ya watu

Mtahiniwa katika sehemu ya hitimisho atoe hitimisho la kazi yake.

**Utangulizi 01**
**Kiini hoja 6@ 03=**
**Hitimisho 01**
**Jumla 20**

8. Katika sehemu ya utangulizi mtahiniwa atoe fasili ya maneno ya msingi na usuli juu ya utawala wa waarabu nchini Tanganyika kabla ya uhuru.

   Katika sehemu ya kiini mtahiniwa aoneshe namna Waarabu walivyodumaza lugha ya kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru

   i. Kuingizwa kwa misamiati mingi
   ii. Kutoisambaza lugha ya Kiswahili maeneo mengi
   iii. Kutochukua hatua za kusanifisha
   iv. Kutotafisiri na kuandika vitabu vya Kiswahili
   v. Matumizi duni ya lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiswahili ilitumiwa sehemu chache na kwa ngazi za chini
   vi. Dharau kwa lugha ya Kiswahili na kuiona ni lugha ya watu wa tabaka la chini na ya makabwela.
   vii. Matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili katika dini ya uislamu na kufungamanishwa na imani za kidini.

   Katika sehemu ya hitimisho, mtahiniwa atoe hitimisho la kazi yake

**Utangulizi 01**
**Kiini hoja 6@ 03=**
**Hitimisho 01**
**Jumla 20**